OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)

SHULE YA SEKONDARI KITANDILILO
P.O.BOX 313
MAKAMBAKO
TAREHE……..

MTSS/FI/VOL1/2021.

JINA LA MWANAFUNZI_____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE KWA WANAFUNZI KIDATO CHA KWANZA 2021

Napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kuingia Kidato cha Kwanza katika **SHULE YA SEKONDARI KITANDILILO** mwaka **2021.Shule itafunguliwa tarehe 11 Januari 2021 hivyo wanafunzi wote wanatakiwa kuripoti siku hiyo bila kukosa.**Nafasi uliyopewa muhimu kwako hivyo huna budi kuijali na kuitumia kwa manufaa yako binafsi, familia na taifa kwa ujumla.

Utakuwa na wajibu wa kusoma kwa bidii, kushiriki kikamilifu katika kazi za mikono na uzalishaji mali, kuishi kwa amani,upendo na ushirikiano na watumishi na wanafunzi wenzako ili kupata elimu kwa maisha endelevu

Shule ya Sekondari Kitandililo ipo katika Halmashauri ya Mji Makambako Kata ya Kitandililo na kijiji cha Kitandililo umbali wa kilometa 32 mashariki mwa Mji wa Makambako. Njia ya kuelekea kiwanda cha karatasi cha Mgololo.

Shule hii ni ya kutwa na daharia(Hostel) kwa wavulana.

Pamoja na barua hii naambatanisha fomu zifuatazo

1. Fomu ya kujiandikisha shuleni
2. Sheria za shule
3. Mahitaji muhimu ya shule ya mwanafunzi
4. Fomu ya ahadi ya mwanafunzi na mlezi/mzazi
5. Fomu ya afya ya mwanafunzi (Ijazwe na daktari wa hospital ya Serikali)

NB: Fomu 1, 4 na 5 zijazwe na zirudishwe shuleni tarehe ya kuripoti

KARIBU SANA KITANDILILO SEKONDARI

…….
ALBERT KAHONGA
MKUU WA SHULE

1. FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULE

A. TAARIFA ZA MWANAFUNZI

i. Jina la mwanafunzi……
ii. Mahali alipozaliwa…….Mkoa……..
iii. Tarehe ya kuzaliwa……
iv. Dini ……...Dhehebu……..
v. Shule ya Msingi ulikotoka……..……..
vi. Shughuli unazopendelea mbali na masomo kama vile mpira wa miguu, mpira wa mkono, riadha, kuimba n.k ……
vii. Sahihi ya mwanafunzi……Tarehe……..

B. TAARIFA ZA WAZAZI

i. Baba yu hai……..... Ndiyo/Hapana Simu…….
ii. Mama yu hai……Ndiyo/Hapana Simu…….
iii. Jina la Mlezi/Mzazi anayekulea……
iv. Uhusiano wako na Mlezi……..
v. Kazi ya Mzazi/Mlezi…….
vi. Anwani ya Mzazi/Mlezi……Simu…….
vii. Mahali ambapo Mzazi/Mlezi anaishi
Kijiji/Mji ……. Kata……. Tarafa …….
Wilaya……. Mkoa ……

Sahihi ya mzazi/mlezi …… Tarehe……

C. NDUGU WENGINE WA KARIBU

JINA	SAHIHI	ANWANI YAKE	SIMU
1. ……	……	……..	……
2. ……	……	……..	……
3. ……	……	……..	……

D. OFISI YA MTENDAJI KATA AU MWENYEKITI WA MTAA/KIJIJI AMBAKO MZAZI AU MLEZI WA MWANAFUNZI ANAISHI.

i. Jina……..
ii. Kata ya ……. Anwani…….
iii. Jina…….Kijiji cha……Anwani……

2. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

Sheria za Shule zina lenga katika kumlea mwanafunzi awe na nidhamu, azingatie maadili ya Taifa letu na hatimaye aishi kama raia mwema anayekubalika na jamii yetu.
Ni imani yetu kuwa shule yenye wanafunzi wenye nidhamu hufanya vizuri katika taaluma.

HIVYO NI LAZIMA KWA KILA MWANAFUNZI WA SHULE HII.

1) Kuhudhuria masomo kila siku, tatizo la ugonjwa, msiba nk litaombewa ruhusa.
2) Kusalimu watu wote na hasa waliomzidi umri
3) Kusimama mwalimu anapoingia darasani au wakati wa kuuliza na kujibu swali.
4) Kuwahi shuleni na kufanya usafi eneo ulilopangiwa
5) Kuvaa nguo za heshima shuleni na hata nyumbani
6) Kutii sheria zote za shule
7) Ni muhimu kutunza usafi wako binafsi na mazingira ya shule
8) Kukaa kimya na nidhamu darasani
9) Usizungumze na mwalimu au mtu anayekuzidi umri ukiwa umekaa, mikono ikiwa mfukoni ama kofia kichwani au ukiwa umevaa miwani ya jua.
10) Mwanafunzi huruhusiwi kutembea usiku bila sababu yoyote hata kama atakuwa kwa wazazi wake.
11) Mwanafunzi asiruhusiwe kufanya sherehe usiku
12) Daima uwe msafi kimwili na mavazi.Uwe na nywele fupi,kufuga ndevu au masharubu hairuhusiwi shuleni.
13) Ni marufuku mwanafunzi kujiunga na vilabu vya michezo nje ya shule
14) Ni marufuku kwa mwanafunzi kushiriki katika vigenge vya usengenyaji au kusema uongo.
15) Usifanye biashara aina yoyote shuleni.
16) Usichelewe siku za kufungua shule au usiongeze siku za ruhusa.
17) Usikatae uteuzi wa kushiriki shughuli za michezo n.k
18) Usigune wakati mwalimu au kiongozi yoyote anapotoa tangazo kama kuna swali nyosha mkono, utaratibu ufuatwe.
19) Usibandike au kuandika tangazo lolote lile bila ruhusa ya mwalimu anayehusika.

NI MARUFUKU KWA MWANAFUNZI

a) Kutumia lugha chafu kama matusi n.k
b) Kutembelea nyumba za kulala wageni au nyumba za walimu, baa, vilabu vya pombe na kumbi za starehe.
c) Kufuga kucha, nywele ndefu, kuvaa mikufu, kupaka marashi au rangi kwenye kucha au kuvaa hereni, kuwa na kamera, redio, simu ya mkononi awapo shuleni.
d) Kufanya mapenzi na wanafunzi wenzake au watu wengine nje na ndani ya shule
e) Kuambatana na makundi ya wahuni wa mitaani
f) Kuondoka shuleni kabla ya muda wa masomo kuisha (utoro).

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI AFUKUZWE SHULE

a) Wizi
b) Uasherati, ubakaji na ushoga
c) Ulevi wa aina yoyote, pombe au madawa ya kulevya
d) Uvutaji bangi
e) Makosa ya jirani
f) Kupigana au kupiga
g) Kuoa au kuolewa
h) kusababisha mimba ndani ya shule au nje shule
i) Kuharibu kwa makusudio mali za umma
j) Kudharau bendera au wimbo wa taifa
k) Kufanya, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au kuhatarisha amani ya shule wakati wowote ule.
l) Kukataa kutii amri ya mkuu wa shule au mwalimu yoyote.

***ZINGATIO*: MAISHA YA SHULE NI MAZURI KWA WALE TU WATAKAOFUATA SHERIA ZA SHULE.**

SHULE ITAFUNGULIWA TAREHE 11/01/2021 SAA MOJA ASUBUHI.FIKA BILA KUKOSA

3. MAHITAJI MUHIMU YA SHULE KWA MWANAFUNZI

SARE ZA SHULE:

A: ***WAVULANA***

i. Mashati mawili meupe (tetron mikono mirefu)
ii. Suruali mbili za heshima rangi sampuli imeambatanishwa,upana wa suruali miguuni isipungue inchi 14.
iii. Soksi jozi mbili rangi nyeusi.
iv. Sweta kijani jeshi nyeusi yenye shingo la "V"
v. Tai mbili za rangi ya suruali.
vi. Viatu vya ngozi vyeusi visivyo na kisigino kirefu vya kufunga na kamba.
vii. Sahani na kijiko kwa ajili ya chakula cha mchana.

B*: SARE YA MICHEZO:*

- **T**racksuit nyeusi yenye ufito mweupe na Tshirt nyeupe
- Raba za michezo
- Bukta nyeusi

ZINGATIO*: *KABLA YA KUPOKELEWA/ KUSAJILIWA UKAGUZI WA SARE UTAFANYIKA.

C: MCHANGO WA CHAKULA CHA MCHANA **(WANAFUNZI WA KUTWA)**

Michango hii ni kwa mwaka:

i. Mahindi debe mbili (debe 2)
ii. Maharage Kilo 20.
iii. Fedha taslimu 30,000/=

MAHITAJI YA MWANAFUNZI ;

I. Daftari kumi kubwa (10)
II. Mkebe (vifaa vya Hisabati / Mathematical Set)
III. Ruler futi moja na kalamu za wino na penseli.
IV. Jembe jipya lenye mpini wa mti sio mwanzi.
V. Ndoo ya lita 10.
VI. Spring file (Plastic)2/ File folder.
VII. Mkoba nadhifu wa kubebea daftari sio vifungashio.
VIII. Fyekeo (lililonolewa) na brooms (fagio) (kwa wanafunzi wa kutwa).
IX. Mopa na fagio laini (kwa wanafunzi wa hosteli)
X. Kamusi ya Kiingereza kwa Kiingereza.

4. FOMU YA AHADI:

1. AHADI YA MZAZI / MLEZI

Mimi …….. Mzazi / Mlezi wa mwanafunzi …… naahidi / siahidi kwamba:

a) Nitashirikiana na kikamilifu na uongozi wa shule, walimu na wafanyakazi wengine katika kumuelimisha na kumlea mtoto wangu. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa anazingatia sheria na taratibu zote za shule na kuyatimiza yote muhimu yaliyotajwa hapo juu.
b) Nitafanya kila niwezalo ili kumuwezesha mwanangu kufika shuleni mapema, kuwa na mazingira mazuri ya kujifunzia na kufaulu kwa muda wote wa miaka minne (04).

Sahihi ya mzazi / mlezi…….. Tarehe:……..

---

2. AHADI YA MWANAFUNZI.

Mimi ……

1. Nimesoma na kuyaelewa maelekezo yote na sheria na taratibu za shule ninakubali/ sikubali kuingia Kidato cha Kwanza katika Shule ya Sekondari ya KITANDILILO kuanzia tarehe …… hadi nitakapohitimu Kidato chaNne.
2. Kwahiyo naahidi / siahidi kwamba.
   a) Nitazitii sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa.
   b) Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na uongozi wa Chama Tawala na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
   c) Nitatunza mali ya umma ambayo ni pamoja na mzingira, samani (furniture), vitabu n.k.

Sahihi ya Mwanafunzi……. Tarehe:……

PRESIDENT'S OFFICE – RALG

KITANDILILO SECONDARY SCHOOL,

P. O. BOX. 313,

MAKAMBAKO.

DATE;……..

REF.NO. KTSS / F.1/_____

THE MEDICAL OFFICER,

…….

…….

RE.**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

Please Kindly examine (name)…….to determine his/ her physical and mental fitness for pursuing Secondary School studies.

…….
ALBERT KAHONGA.
HEADMASTER.

1. Eye sight ……..
2. Hearing …….
3. Speech ……..…
4. Limbs ……
5. Leprosy ……
6. Epilepsy ……..
7. Cardiac disease ……
8. Rheumatism …….
9. Venereal diseases …….
10. Pregnancy (for girls) …….
11. Any other serious diseases ……

I certify that the above named fit/ unfit to pursue his/her studies as required:

Designation ……
Station ……
Signature ……..
Date …….
Stamp ……

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)
SHULE YA SEKONDARI KITANDILILO.

Wanafunzi wa Hosteli (DAHARIA)

Shule ya Sekondari Kitandililo inawakaribisha wanafunzi wote wanaopenda kukaa hosteli

MAHITAJI MUHIMU

- Mahindi debe (10)
- Maharage debe tatu (03)
- Mchele kilogram ishirini (20)
- Fedha ya chakula taslimu 120,000/=
- Ujenzi/Ukarabati 20,000/=
- Karatasi (ream) bunda 01
- Fedha ya matibabu 10,0000/=
- Fedha kwa ajili ya tahadhari 10,000/=

  N B Mahindi, maharage, mchele, fedha ya chakula vinaweza kuchangiwa nusu yake kwa ajili ya nusu mhula.

MAHITAJI BINAFSI

- Tracksuit nyeusi yenye mistari myeupe
- Nguo za kuvaa jioni baada ya masomo na mwisho wa wiki
  (Suruali darkblue na Tshirt nyeupe)
- Tranka (mzinga) la bati la kuhifadhia vitu vyake
- Godoro futi mbili na nusu (ft 2½) au (atakodishwa shuleni kwa 10, 000/= kwa mwaka) kwa watakaowahi
- Sahani, kikombe na kijiko
- Shuka mbili rangi ya pink na blanketi dogo jepesi.
- Ndoo ya kuogea
- Taulo, Mswaki, mafuta, kandambili, sabuni,

N;B Mwanafunzi yeyote hataruhusiwa kuja na nguo au mavazi ya nyumbani ambayo hayajatajwa kwenye orodha hii, Muda wote mwanafunzi atatakiwa kuvaa sare ya shule tu.

Hosteli inaongozwa kwa sheria kanuni na taratibu mbalimbali hivyo zinatakiwa kuzingatiwa na kila mwanafunzi. Kinyume chake mwanafunzi atapoteza sifa za kukaa hosteli.

……
ALBERT KAHONGA
MKUU WA SHULE.